OFISI YA RAIS TAMISEMI
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA, NA UFUNDI
HALMASHAURI YA MJI MBINGA

SHULE YA SEKONDARI DR.AM SHEIN,
S.L.P 461,
MBINGA.
Mob: 0627544280

Kumb NA ED/DSS/UT/27
Jina la mwanafunzi .....
Shule.....
S,l,p .....
Mbinga

YAH: MAAGIZO YAA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI DR.AM.SHEIN HALMASHAURI YA MJI MBINGA, MKOA WA RUVUMA MWAKA 2020

1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari Dr.A.M Shein ipo mpepai umbali wa kilometa 34 kutoka makao makuu ya Halmashauri ya mji wa mbinga. Muhula wa masomo utaanza tarehe 11/01/2021 unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti shuleni ni tarehe 11/01/2021

2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1 Sare za Shule

a. Sare ya Shule hii ni suruali mbili aina ya kaki kwa wavulana na wasichana sketi mbili rangi ya kijani (rangi ifunane na kitambaa kilichobandikwa hapo juu) maelezo ya mshono kwa wavulana ni suruali mifuko miwili pembeni na mfuko mmoja nyuma na iwe na malinda mawili. tafadhali suruali nyembamba chini (yaani modo) hairuhusiwi, mashati meupe mikono mifupi mawili. Kwa wasichana sketi rinda boksi urefu wa sketi ivuke magoti na mashati meupe mikono mifupi mawili
b. Masweta pea mbili rangi ya kijani kwa wavulana na wasichana
c. Viatu pea mbili nyeusi vya ngozi vyenye kamba na visigino vifupi, soksi nyeupe pea mbili kwa wasichana na wavulana soksi nyeusi pea mbili.
d. Sare ya michezo kwa shule hii ni traksuti kwa wasichana Rangi nyeusi na wavulana rangi nyekundu
e. Sare ya kazi ni zambarau kwa wasichana gauni (shamba dress)

2.2 Pamoja na maagizo ya hapo juu unatakiwa kuja na vifaa utakavyotumia katika kusoma/kujifunza kwako. Vifaa hivyo ni pamoja na

i. Daftari kumi (10) aina ya Counter Book au Zaidi.
ii. Daftari kumi ndogo aina ya msomi.
iii. Kalamu za wino za kutosha, Penseli HB, rula na mkebe wa hesabu pamoja na
iv. Begi la kubebea daftari.

2.3. Suala la chakula cha asubuhi na mchana cha mwanafunzi awapo shuleni ni jukumu la mzazi

2.4. Mzazi/mlezi unatakiwa kumpatia mahitaji mengine muhimu ya kibinadamu mtoto wako kama vile fedha za matumizi (pocket money) n.k.

2.5. Shule hii haina bweni. Hivyo ikiwa mtoto anatoka mbali na shule, mzazi unashauriwa kumtafutia mtoto wako makazi salama ya kuishi jirani na shule. Hakikisha mtoto wako unamtengenezea mazingira mazuri ya kujisomea ikiwa ni pamoja na kumwandalia kitanda, godoro, shuka, blanketi, ndoo ya kuogea na taa ya kujisomea awapo nyumbani.

3.0. Sheria na kanuni muhimu za shule hii:-

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu na .25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria na. 10 ya mwaka 1995 Aidha nazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi, yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Raisi – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo mara baada ya kulipoti shuleni:

a) Heshima kwa viongozi, wazazi,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation).
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maaelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii:
f). Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
g). Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
h). Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
i). Kutunza mali za umma.

3.4. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule:-

a) Wizi.
b) Uasherati na ushoga.
c) Ubakaji.
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k.
e) Kupiga au Kupigana.
f) Kuharibu makusudi mali ya umma.
g) Kudharau Bendera ya Taifa.
h) Kuwa mjamzito/kupata mimba au kusababisha mimba
i) Kuoa na kuolewa
j) Kutoa mimba.
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
l) Kuwa na simu ya mkononi.

4.0. Mambo mengine muhimu yanapaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi:

a) Medical Examination form ijazwe na mganga mkuu wa hospitali ya serikali (Hospitali ya Wilaya ya Mbinga/Mbuyula) na ukabidhi kwa mkuu wa shule siku ya kuripoti, zingatia fomu za afya zisijazwe kwenye kituo cha afya, zahanati au hospitali yoyote za misheni mfano Litembo, peramio au Hospitali ya masista Mbinga. Fomu isiyojazwa kwenye hospitali ya wilaya Mbinga/Mbuyula na kusainiwa na mganga mkuu itakuwa batili na haitapokelewa.
b) Fomu ya ahadi ya kuhudhuria masomo.

5.0. Tafadhari soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.
NB. Shule haitamvumilia mwanafunzi atakayekiuka kanuni hizo hapo juu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

.....
MILLINGA W.H
MKUU WA SHULE

THE HEADMASTER
DR. A. M. SHEIN SECONDARY SCHOOL
P. O. BOX 451 MBINGA

OFISI YA RAISI TAMISEMI
SHULE YA SEKONDARI DR. A.M SHEIN
AHADI YA KUHUDHURIA MASOMO

A. MWANAFUNZI

I. **JINA KAMILI** .....
II. Shule ya msingi uliyosoma.....
III. Namba ya mtihani .....
IV. Tarehe ya kuzaliwa .....
V. Naahidi kuwa nitahudhuria masomo muda wote wa miaka minne
VI. Naahidi kufuata sheria zote za shule
VII. Sahihi ..... tarehe .....

B. AFISA MTENDAJI WA KIJIJI

i. Jina kamili .....
ii. Kijiji .....kata .....
iii. Nathibitisha kuwa mwanafunzi .....ni wa kijiji hiki na ni raia wa Tanzania/si raia wa Tanzania naahidi kijiji kitahakikisha kuwa anasoma na kumaliza masomo yake
iv. Sahihi.....muhuri.....tarehe.....

C. MZAZI/MLEZI

Jina.....

a. Nakubali mwanafunzi apate elimu yake shule ya sekondari DR.AM SHEIN
b. Na kwamba atafuata sheria na maelekezo yote,Vinginevyo aadhibiwe
c. Na kwamba mwanafunzi alelewe katika dini/dhehebu la .....
d. Na kwamba haruhusiwi kuwa na simu
e. Na kwamba nitatekeleza maagizo yote yaliyoainishwa katika fomu hii
f. Sahihi ya mzazi/ mlezi ..... tarehe .....

.....
MILLINGA W.H
MKUU WA SHULE

THE HEADMASTER
DR. A. M. SHEIN SECONDARY SCHOOL
P. O. BOX 451 MBINGA

THE UNITED PUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF EDUCATION AND VOCATIONAL TRAINING
MBINGA DITRICT COUNCIL

DATE .....

TO:

The Medical Officer,
.....
.....
.....

RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Please Examine .....as to his /her physical and mental fitness for admission as a form ..... student at ..... school.

Your sincerely,
.....
THE HEAD MASTER

THE HEADMASTER
DR. A. M. SHEIN SECONDARY SCHOOL
P. O. BOX 451 MBINGA

The Headmaster;
I have examined ..... and consider that he/she is physical and mentally fit for admission to pursue a full course of secondary school.

1. Blood Pressure .....Haemoglobin .....Blood group.....
2. EYE
   Visual acuity, with/without glasses Right .....Left .....
3. ENT
   Hearing (a)Right Ear.....(b)Left Ear.....
   Throat.....Nose.....(c) Speech .....
4. Respiratory system
   (a)TB..... (B)Asthma.....
5. CVS
   (a)Any Congenital heart disease.....
6. GIT
   (a)PUD..... (b)Stool.....
7. GUS
   (a)Venereal disease (i) VDRL.....
   (b)Urinalysis.....(c) Pregnant test.....
8. RES (a) Skin diseases..... (b) Any Allergy.....
9. MMS (a) Any deformity.....(b)Any chronic illness of the joints.....

10. Are there serious disease eg. Leprosy, Epilepsy, Diabetes?
Specify.....

11. General comments.....
.....

DATE .....

STATION .....

SIGNATURE ..... **DESGNATION** .....

Approved By:

....

TOWN MEDICAL OFFICER. **DATE**

MBINGA TOWN COUNCIL